## MAELEZO YA MAZAZI/ MLEZI HAYA YASOMWE KWA MAKINI NA MWANAFUNZI

1. Unafahamishwa kwamba umechaguliwa kujiunga na Chuo cha Ufundi cha KIHONDA RVTSC **BWENI** (BOARDING) Level I katika fani ya .......................................na kwamba hakutakuwepo na uwezekano wa kubadili fani uanzapo masomi.
2. Mafunzo yatachukua muda wa miaka mitatu (3)

2.1 Mafunzo yatatolewa na pande mbili; wiki 20 utakuwa chuo na wiki 32 utakuwa kiwandani/eneo la kazi kwa mwaka.

2.2 Mzazi/mlezi atagharamia malazi na chakula wakati wote ukiwa kiwandani/sehemu za kazi

3. Mafunzo yaataanza rasmi tarehe 15/01/2024
4. Unatakiwa kuthibitishwa na daktari wa serikali kuwa unayo afya nzuri ya kumudu mafuzno katika fani uliyopangiwa
5. Unatakiwa kuthibitisha wewe mwenyewe na mzazi / mlezi /mdhamini wako kwamba unakubali nafasi ya mafunzo uliyopangiwa.
6. Unatakiwa kununua vifaa vifuatavyo kwa matuzmizi yako chuoni

6.1 Mashati mawili meupe (mikono mifupi ) ya Tetroni

6.2 Jozi moja ya viatu vyeusi , vya ngozi visigino vifupi

6.3 sweta moja kwa ajili ya baridi lenye rangi ya “Dark Blue”mikono mirefu

6.4 Uje na picha tatu (passport size)

6.5 Vifaa vya hesabu na kuchorea (mathematical set)

6.6 Daftari nane (8) kubwa (COUNTER BOOK Q3)

6.7 Uje na rimu moja ya karatasi nyeupe A4 size

6.8 Uje na fyekeo moja kwa wanafunzi wa fani ya zana za kilimo (agro mechanics) leta jembe na mpini badala ya fyekeo.

6.9 Umepatiwa nafasi ya bweni, uje mashuka (rangi ya pink kwa wasichana na laiti bluu kwa wavulana), kikombe, kijiko sahani neti ya kuzuia mbu na ndoo ya lita kuni

6.10 Uje naTruki suti kwa kwa ajili ya michezo (rangi daki bluu)

6.11 Uje suruali ya kitambaa vyeusi na fulana(T shirt) ya rangi ya daki bluu, kwa ajili ya matumizi ya kawaida

7. a) Jedwali la gharama za chuo

| Na | MUHULA I | | MUHULA WA II | |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Bima ya afya afya ( NHIF | 50,400)/= | Ada ya mafunzo | 60,000/= |
| 2 | Fedhaya ukarabati | 10,000/= | Mahafali | 20,000/= |
| 3 | Kitambulisho cha Chuo | 5,000/= | Ada ya mtihani | 25,000/= |
| 4 | Michezo | 10,000/= | - | |
| 5 | Nembo ya VETA | 5,000/= | - | |
| 6 | Ada ya mafunzo | 60,000/= | - | |
| 7 | T-shirt | 20,000/= | - | |
| 8 | Viatu vya usalama | 55,000/= | - | |
| 9 | Suruali mbili za dark blue | 50,000/- | - | |
| 10 | Ovaroli la dark blue | 30,000 | - | |
| 11 | Godoro (Kukodisha) | 15,000 | | |
| | **Jumla kuu** | **310,400/=** | | **105,000/=** |

**NAMNA YA KULIPA MALIPO YOTE**

b) ada ya mafunzo ni Tshs **120,000/=** kwa mwaka, unaweza kulipa nusu ada Tshs **60,000/=** uje nazo chuoni utapewa “control number” ya kulipia mara ufikapo chuoni.

c) fedha zote zilizobaki zilipwe kwa mkupuo mmoja , kiasi cha Tshs **235,400** /= kwa asiye na kadi ya **BIMA** ya afya .Mwenye kadi ya Bima alipe Tshs **185,000/=** .Fedha hizi aje nazo chuoni atapewa control number ya kulipia

hutapokelwa chuoni iwapo utafika bila kutekeleza vifungu vilivyotajwa hapo juu .Fedha ikishalipwa **hairudishwi**

8. unatakiwa kufuata sheria na taratibu zote za chuoni zilizoambatanishwa kwenye barua
9. unatakiwa kufika chuoni na barua hii siku ya kuanza mafunzo. Wanafunzi wanapokelewa chuoni muda wa saa za kazi. Mwisho wa kuingia chuoni ni saa 9:30 jioni
10. nafasi yako itapotea kama utashindwa kuripoti ndani ya wiki mbili , tarehe **15/01/2024** baada ya tarehe ya kufungua chuo, yaani tarehe **29/01/2024**

**MAELEZO MENGINE UTAELEZWA UFIKAPO CHUONI**

**Viambatisho:-**

1. Sheria Za Chuo
2. Medical Examination Form

## SHERIA ZA CHUO KWA WANACHUO WA KUTWA NA BWANI

CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI NA HUDUMA BOX 2208 (KIHONDA WING) MOROGORO

Ili kufanikisha mafunz ya awali ya ufundi stadi kila mwanachuo anatakiwa kufuata sheria zifuatazo

**1.0 Mahudhurio :**

1.1 kila mwanafunzi anatakiwa kufika chuoni saa 1: 15 asubuhi na awe amesimama foleni ifikapo saa 1:30 adhabu kali itatolewa kwa wachelewaji

1.2 mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya chuo kwenda nyumbani, hospitali au sehemu nyingine yoyote bila kuruhusiwa na mwalimu (mkuu wa karakana)

1.3 mwanafunzi apatapo matatizo ya msiba , kuugua au kuuguliwa ni lazima taarifa zifikishwe ofisini vinginevyo atahusishwa na kosa la utoro ambalo litafuatiwa na adhabu

1.4 mahudhurio chini ya 85%mwanafunzi atanyimwa cheti cha kuhitimu mafunzo

**2.0 Mavazi:**

2.1 sare ya chuo ni suruali ya bluu na shati jeupe la mikono mifupi ambalo wakati wote liwe limechomekewa

2.2 ovaroli livaliwe wakati wa vipindi vya kazi za mikono (practical) tu.

2.3 Viatu vyenye visigino virefu (raison) na kandambili (sandals) haviruhusiwi kuvaliwa chuoni

2.4 Hairuhusiwi kwenda na sare za chuo sehemu za starehe kama vile baa, kumbi za miziki na sehemu nyingine zinazolingana na hizo.

**3.0 Usafi wa mwili**

3.1 Hairuhusiwi kuvaa heren,pete, bangili na mapambo ya aina yoyote katika kipindi chote cha mafunzo.

3.2 Hairuhusiwi kutumia vipodozi au manukato yanayotoa harufu kiasi cha kusumbua watu wengine na kushindwa kufuata masomo. Kupaka rangi mdomo (lip stic) na kupaka rangi kucha hairuhusiwi kabisa

**3.3 Nywele kw awavulana**

3.3.1 Zikatwe fupi na mitindo kama PANK, AMERICAN BASE na KIPARA haviruhusiwi kabisa

3.3.2Ndevu haziruhusiwi

**3.4 Nywele kwa wasichana**

3.4.1Zikatwe / ziwe fupi au zisukwe kwa mistari (twende kilioni)

***NB**: Nywele ndefu na nywele zenye kupakwa madawa kama vile curl, rsata na golden hair haziruhusiwi kabisa kwakipindi chote cha mafunzo.*

**4.0 wizi wa mali**

4.1 vitendo vyote vya wizi haviruhusiwi,pindi ikibainika mwanafunzi ameiba mali ya chuo au ya mwanafunzi mwenzake au mfanyakazi wa Chuo , basi atafukuzwa chuo mara moja

4.2 ukipoteza vifaa vya chuo utatakiwa kulipa gharama kamili ya kifaa ua ukanunue kifaa chenyewe au ulete badala ya ulichopoteza.

4.3 Hairuhusiwi mwanafunzi kuingia na kifaa kutoka karakana na wakati wa kutoka getini

4.4 Mwanafunzi atapekuliwa wakati wa kutoka karakana na wakati wa kutoka getini

**5.0 Ugomvi**

5.1 Ugomvi ,kupigana au kushambuliana ni makosa ya jinai,atakayepatikana akijihusisha na mtendo ya namna hiyo atafukuzwa chuoni na kukabidhiwa vyombo vya dola.

**6.0 Ulevi**

6.1 Iwapo itabainika kuwa mwanafunzi analewa, au kuonekana katika sehemu za vileo ,anavuta sigara, bangi au anatumia madawa ya kulevya adhabu yake ni kufukuzwa chuo mara moja.

**7.0 Mapenzi**

7.1 Uhusiano wa kimapenzi chuoni kati ya mwanafunzi na mwanafunzi au kati ya mfanyakazi na mwanafunzi hauruhusiwi kabisa.7.2 Mwanachuo akiwa na mimba hataruhusiwa kuendelea na masomo

7.3 Mwanafunzi wa kiume au wa kike haruhusiwi kabisa kuingia katika maeneo wanamoishi watumishi bila kibali au ruhusa.

**8.0 Migomo**

8.1 migomo ni marufuku : na kuchochea migomo ni kosa lisilostahilimika hivyo atakayehusika au kusababisha migomo atafukuzwa chuo mara moja.

**9.0 Lugha**

9.1 Lugha inayotumika kuendeshea maosmo ni kiingereza hivyo ni wajibu wa kila mwanachuo kujifunza kiingereeza kwa bidii.

**10.0 Kubadilisha jina**

Jina lisibadilishwe mpaka ziwepo sababu za kutosha na hati maalum kwa uthibitisho ;mkuu wa chuo ajulishwe mara moja hatua zote za kubalisha jina la mwanafunzi.

10.1 hairuhusiwi mwanafunzi kuingia na simu darasani au karakana.

**VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING AUTHORITY**

The medical officer,

................................................

................................................

................................................

..................................................

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

Please examine the above named candidate to his /her fitness to undergo training and subsequently work as a/an..........................................................................................

i) Eyesight ......................................................................................

ii) Hearing ......................................................................................

iii) Asthma ......................................................................................

iv) Other serious disease.........................................................................

**MEDICAL CERTIFICATE**

I exanimated the above named and consider that he/she is physically / unit for

training. Date..................................................Designation..........................................

---

**KUKUBALI NAFASI YA MAFUNZO YA UFUNDI STADI**

**a) MWANACHUO**

Mimi ......................................................ninakubali nafasi ya mafunzo niliyopangiwa pamoja na kuzingatia sheria na kanuni za chuo.

Sahihi..............................................Tarehe ................................................

**b) MDHAMINI**

Mimi ..............................................S.L.P.........................................................

Sahihi..............................................Tarehe ..................................................